JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

NA. 7 YA 1993

NINAKUBALI,

.....................................
*Rais*

11 June 1993

**Sheria ya kufanya mabadiliko katika masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kutoa madaraka kwa Tume ya Uchaguzi, kusimamia na kuratibu uchaguzi wa Madiwani pamoja na mambo mengine yanayoambatana nayo**

[ ............................................ ]

**1.** Sheria hii iitwe Sheria ya Mabadiliko ya Kumi katika Katiba ya Nchi ya mwaka 1993.

**2.** Ibara ya 74 inafanyiwa mabadiliko katika—

(a) ibara ndogo ya (3) kwa kuweka mkato na kuongeza neno "Diwani" mara baada ya neno "Mbunge";

(b) ibara ndogo ya (6) kwa kuongeza aya mpya zifuatazo—

"(d) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa uchaguzi wa madiwani;

(e) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge".

Imepitishwa na Bunge tarehe 23 Aprili, 1993

G. F. MLAWA,
*Katibu wa Bunge*

Imepigwa Chapa na Mpigachapa wa Serikali, Dar es Salaam—Tanzania